TANGAZO LA SERIKALI NA. 606 la tarehe 25/8/2023

SHERIA YA VIWANGO,
(SURA YA 130)

# NOTISI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 20 (2))*

NOTISI YA KUSUDIO LA KUTANGAZA VIWANGO VYA LAZIMA
YA MWAKA 2023

Jina

1. Notisi hii itajulikana kama Notisi ya Kusudio la Kutangaza Viwango vya Lazima ya Mwaka 2023.

Kusudio la kutangazwa kwa viwango

2. Umma unataarifiwa kuwa, Shirika linakusudia kupendekeza kwa Waziri kutangazwa kwa Viwango vilivyoanishwa kwenye Jedwali.

Pingamizi

3. Mtu yeyote mwenye pingamizi lolote kuhusiana na Viwango vilivyoainishwa kwenye Jedwali anaweza kuwasilisha pingamizi hilo kwa maandishi katika Ofisi ya Shirika ndani ya siku sitini kuanzia tarehe ya kutangazwa kwa Notisi hii.

JEDWALI

*(Imetengenezwa chini ya aya 2)*

| Na. | NAMBA YA KIWANGO | JINA LA KIWANGO KWA KISWAHILI | AINA YA KIWANGO |
| --- | --- | --- | --- |

*Tangazo La Serikali Na. 606 (Linaendelea)*

| Na. | NAMBA YA KIWANGO | JINA LA KIWANGO KWA KISWAHILI | AINA YA KIWANGO |
|---|---|---|---|
| 1. | TZS 3654/ISO 23875:2021 | Uchimbaji madini - Mifumo ya udhibiti wa ubora wa hewa kwa funga za waendeshaji - Mahitaji ya utendaji na mbinu ya majaribio | Lazima |
| 2. | TZS 3656 | Sifa za Makaa ya mawe kwa Matumizi ya Viwandani | Lazima |
| 3. | TZS 3669 | Mavazi ya kinga kwa ajili ya matumizi katika mchakato wa kulehemu na washirika | Lazima |
| 4. | TZS 3670 | Nguo za ulinzi dhidi ya joto na moto - Mapendekezo ya jumla ya uteuzi, utunzaji na matumizi ya nguo za kinga | Lazima |
| 5. | TZS 3676 | Nguo - vipimo vya Turubai isiyopitisha maji iliyotengenezwa kutoka kwa vitambaa vya polyester vilivyofumwa | Lazima |
| 6. | TZS 3677 | Nguo - Neti za michezo - Matakwa | Lazima |
| 7. | TZS 3679 | Nguo - matakwa ya kamba za jute | Lazima |
| 8. | TZS 3664-1/ISO 22982-1:2021 | Ufungashaji wa usafirishaji -Vifurushi vya usafiri vinavyodhibitiwa na halijoto kwa usafirishaji wa vifurushi -Sehemu ya 1: Mahitaji ya jumla | Lazima |

Dar es salaam
11 Agositi, 2023

ATHUMAN Y. NGENYA
*Mkurugenzi Mkuu*